ISSN 0856 - 0331X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

# *ACT SUPPLIMENT*

**No. 5** **22nd April, 2005**

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 16 Vol. 86 dated 22nd April, 2005*

Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of Government

## SHERIA YA MABADILIKO YA KUMI NA NNE KATIKA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO YA MWAKA 1977

---

YALIYOMO

---

*Ibara* *Kichwa cha Habari*

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

1. Jina la Sheria.

SEHEMU YA PILI
KUFANYA MABADILIKO KWENYE KATIBA

2. Kufanya mabadiliko katika Katiba.
3. Kufanya mabadiliko katika UTANGULIZI.
4. Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 3.
5. Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 18.
6. Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 19.
7. Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 20.
8. Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 21.
9. Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 24.
10. Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 37.
11. Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 59.
12. Kuongeza Ibara mpya za 59A na 59B.
13. Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 66.
14. Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 74.
15. Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 78.
16. Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 107A.

17. Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 109.
18. Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 110.
19. Kuongeza Ibara mpya ya 110A.
20. Kufanya mabadiliko katika Sehemu ya Tatu ya Sura ya Tano.
21. Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 116.
22. Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 118.
23. Kufanya mabadiliko katika Ibara 120.
24. Kuongeza Ibara mpya ya 120A.
25. Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 151.

**Na. 1 ya 2005**

**Nakubali**
BENJAMIN W. MKAPA,
**Rais**
**6 Aprili, 2005**

**Sheria ya Mabadiliko ya Kumi na Nne Katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

IMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

**1.** Sheria hii itaitwa Sheria ya Mabadiliko ya Kumi na Nne Katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka, 2005. Jina la Sheria

SEHEMU YA PILI
KUFANYA MABADILIKO KATIKA KATIBA

**2.** Masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya Mwaka 1977, ambayo katika mafungu yafuatayo ya Sheria hii itaitwa kwa kifupi "Katiba", yanabadilishwa kwa namna ilivyoelezwa katika vifungu vya Sheria hii. Kufanya mabadiliko katika Katiba

**3.** Sehemu ya "UTANGULIZI" katika Katiba inayohusu "MISINGI YA KATIBA" inafanyiwa mabadiliko kwa kufuta nukta mwishoni mwa aya ya tatu na kuongeza maneno "na isiyokuwa na dini". Kufanya mabadiliko katika Utangulizi

**4.** Ibara ya 3 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko katika ibara ndogo ya (1) kwa kuweka maneno "isiyokuwa na dini," mara baada ya neno "kijamaa". Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 3

Kufanya Mabadiliko katika Ibara ya 18

**5.** Ibara ya 18 ya Katiba inafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

**18.** Kila mtu:

"Uhuru wa maoni

(a) anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake;

(b) anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi;

(c) anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake; na

(d) anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii."

Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 19

**6.** Ibara ya 19 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko:

(a) kwa kuifuta Ibara ndogo ya (2) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(2) Kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa ni huru na jambo la hiari ya mtu binafsi, na shughuli na uendeshaji wa jumuiya za dini zitakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya nchi."

(b) kwa kuongeza Ibara ndogo ya (3) mara tu baada ya Ibara ndogo ya (2) kama ifuatavyo:

"(3) Hifadhi ya haki zilizotajwa katika ibara hii itakuwa chini ya taratibu zilizowekwa na sheria ambazo ni muhimu katika jamii ya kidemokrasia kwa ajili ya usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii na umoja wa kitaifa."

(c) kwa kuitaja Ibara ndogo ya (3) iliyopo kuwa Ibara ndogo ya (4).

Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 20

**7.** Ibara ya 20 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko:

(a) kwa kuifuta Ibara ndogo ya (1) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(1) Kila mtu anao uhuru wa kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika, kushirikiana na watu wengine, na kwa ajili hiyo kutoa mawazo yake hadharani na

kuanzisha na kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo."

(b) kwa kuifuta Ibara ndogo ya (2) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(2) Bila ya kujali masharti ya Ibara ndogo ya (1) na ya (4), haitakuwa halali kwa chama chochote cha siasa kuandikishwa ambacho kutokana na katiba au sera yake-

(a) kinakusudia kukuza au kupigania maslahi ya

(i) imani au kundi lolote la dini;

(ii) kundi lolote la kikabila, mahali watu watokeapo, rangi au jinsia;

(iii) eneo fulani tu katika sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano;

(b) kinapigania kuvunjwa kwa Jamhuri ya Muungano;

(c) kinakubali au kupigania matumizi ya nguvu au mapambano kama njia za kufikia malengo yake ya kisiasa;

(d) kinapigania au kinakusudia kuendesha shughuli zake za kisiasa katika sehemu moja tu ya Jamhuri ya Muungano;

(e) hakiruhusu uongozi wake kuchaguliwa kwa vipindi na kwa njia za kidemokrasia."

(c) kwa kuifuta Ibara ndogo ya (4) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(4) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kulazimishwa kujiunga na chama chochote au shirika lolote au kwa chama chochote cha siasa kukataliwa kusajiliwa kwa sababu tu ya itikadi au falsafa ya chama hicho".

**8.** Ibara ya 21 inafanyiwa mabadiliko katika Ibara ndogo ya (1) kwa kufuta maneno "ya 5," yaliyopo kwenye mstari wa kwanza na kisha kuweka maneno "ya 47" mara baada ya tarakimu ya "39". Kufanya Mabadiliko katika Ibara ya

Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 24

**9.** Ibara ya 24 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuifuta Ibara ndogo ya (1) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"Haki ya kumiliki mali

(1) Kila mtu anayo haki ya kumiliki mali, na haki ya hifadhi ya mali yake aliyonayo kwa mujibu wa sheria."

Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 37

**10.** Ibara ya 37 inafanyiwa mabadiliko-

(a) katika ibara ndogo ya (2) kwa kufuta tarakimu "(3)" inayoonekana kwenye mstari wa mwisho na kuweka badala yake tarakimu "(5)".

(b) kwa kufuta maneno ya utangulizi katika ibara ndogo ya (3) na kuandika upya kama ifuatavyo:

"(3) Endapo Rais atakuwa hayupo katika Jamhuri ya Muungano au atashindwa kutekeleza majukumu yake kwa sababu nyingine yoyote, kazi na shughuli za Rais zitatekelezwa na mmojawapo ya wafuatao kwa kufuata mpangilio ufuatao, yaani-"

(c) kwa kufuta ibara ndogo ya (4) na kuandika upya kama ifuatavyo:

"(4) Endapo Waziri Mkuu ndiye atatekeleza kazi na shughuli za Rais kutokana na sababu kwamba Makamu wa Rais hayupo basi Waziri Mkuu ataacha kutekeleza kazi na shughuli hizo endapo lolote kati ya mambo yafuatayo likitokea mwanzo-

(a) Rais atakaporejea katika Jamhuri ya Muungano au atakapopata nafuu kutokana na maradhi na kuanza kutekeleza kazi za Rais;

(b) Makamu wa Rais atakaporejea katika Jamhuri ya Muungano."

(d) Kwa kuongeza katika ibara ndogo ya (6) maneno "au hawezi kumudu kazi zake" mara baada ya maneno "Jamhuri ya Muungano yaliyopo katika maneno ya utangulizi".

Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 59

**11.** Ibara ya 59 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuifuta ibara ndogo ya (2) na kuiandika upya kama ifuatavyo-

"(2) Mwanasheria Mkuu wa Serikali atateuliwa kutoka miongoni mwa watumishi wa umma wenye sifa ya kufanyakazi za wakili au watu wenye sifa ya kusajiliwa kuwa wakili na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi na tano."

Kuongeza Ibara mpya za 59A na 59B

**12.** Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuongeza Ibara za 59A na 59B mara tu baada ya Ibara ya 59 kama ifuatavyo:

"Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali

59A.-(1) Kutakuwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakayeteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye sifa zilizoainishwa katika ibara ndogo ya (2) ya Ibara ya 59 na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi.

(2) Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwa msaidizi mkuu katika kutekeleza kazi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali na atafanya kazi nyingine kama atakavyoelekezwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali."

59B.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye atateuliwa na Rais, kutoka miongoni mwa watu wenye sifa zilizoainishwa katika ibara ndogo ya (2) ya Ibara ya 59 na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi.

(2) Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa na uwezo wa kufungua, kuendesha na kusimamia mashtaka yote nchini.

(3) Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mujibu wa ibara ndogo ya (2) yaweza kutekelezwa na yeye mwenyewe au kwa maelekezo yake na maofisa waliopo chini yake, au wengineo wanaotekeleza kazi hizo kwa maelekezo yake.

(4) Katika kutekeleza mamlaka yake, Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa huru, hataingiliwa na mtu yeyote au na mamlaka yeyote na atazingatia mambo yafuatayo-

(a) nia ya kutenda haki;
(b) kuzuia matumizi mabaya ya taratibu za utoaji haki; na
(c) maslahi ya umma.

(5) Mkurugenzi wa Mashtaka atatekeleza mamlaka yake kama ilivyoelekezwa katika sheria yoyote iliyotungwa au itakayotungwa na Bunge."

Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 66

**13.** Ibara ya 66 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko katika ibara ndogo ya (1):

(a) kwa kuifuta aya ya (b) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(b) Wabunge wanawake wa idadi isiyopungua asilimia thelathini ya wabunge wote waliotajwa katika aya za (a), (c), (d), (e) na (f) wenye sifa zilitajwa katika Ibara ya 67 watakaochaguliwa na vyama vya siasa kwa mujibu wa Ibara ya 78, na kwa kuzingatia masharti ya uwiano wa kura;"

(b) kwa kuifuta aya ya (e) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(e) Wabunge wasiozidi kumi walioteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye sifa zilizotajwa katika aya za (a) na (c) za Ibara ya 67 na angalau Wabunge watano kati yao wakiwa wanawake;"

(c). kwa kuongeza aya ya (f) mara baada ya aya ya (e) kama ifuatavyo:

"(f) Spika, iwapo hatakuwa amechaguliwa kutoka miongoni mwa Wabunge"

**14.** Ibara ya 74 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko:

Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 74

(i) katika ibara ndogo ya (1) kwa kuifuta aya ya (a) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

(a) Mwenyekiti ambaye atakuwa ni Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani au ni mtu mwenye sifa ya kuwa wakili na amekuwa na sifa hizo kwa muda usiopungua miaka kumi na tano;

(b) Makamu wa Mwenyekiti ambaye atakuwa ni Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani au ni mtu mwenye sifa ya kuwa wakili na amekuwa na sifa hizo kwa muda usiopungua miaka kumi na tano."

**15.** Ibara ya 78 inafanyiwa mabadiliko kwa kuifuta ibara ndogo ya (1) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 78

"(1) Kwa madhumuni ya uchaguzi wa Wabunge wanawake waliotajwa katika ibara ya 66(1)(b), vyama vya siasa vilivyoshiriki katika Uchaguzi Mkuu kwa kufuata utaratibu uliowekwa, na kupata angalau asilimia tano ya kura zote halali za wabunge, vitapendekeza kwa Tume ya Uchaguzi majina ya wanawake kwa kuzingatia uwiano wa kura ambazo kila chama kimepata katika uchaguzi wa Wabunge.

(2) Bila kujali masharti ya ibara ndogo ya (1), zifuatazo zitahesabiwa kuwa ni kura halali za Mbunge aliyepita bila kupingwa katika jimbo la uchaguzi:

(a) endapo chama kimemsimamisha mgombea Urais, kura zilizopigwa katika jimbo kwa mgombea Urais wa chama cha Mbunge huyo; au

(b) endapo chama hakikumsimamisha mgombea Urais, asilimia hamsini na moja ya kura za watu wote waliojiandikisha kupiga kura katika jimbo hilo."

Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 107A

**16.** Ibara ndogo ya (1) ya Ibara ya 107A inafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

"(1) Mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama".

Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 109

**17.** Ibara ya 109 inafanyiwa mabadiliko kwa:-

(a) kufuta ibara ndogo ya (1) na ya (2) na kuandika badala yake ibara ndogo ifuatayo:"

"Majaji wa Mahakama Kuu na uteuzi wao

109.-(1) Kutakuwa na Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu (ambaye katika Ibara zifuatazo kwenye Katiba hii atatajwa tu kwa kifupi kama "Jaji Kiongozi") na Majaji wengine wa Mahakama Kuu wasiopungua thelathini watakaoteuliwa na Rais baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi wa Mahakama."

(b) kuzitaja upya ibara ndogo za (3), (4), (5), (6), (7), (8), (9), (10), (11) na (12) kuwa (2), (3), (4), (5), (6), (7), (8), (9), (10) na (11).

(c) kuzifuta tarakimu (3) na (4) zilizomo katika mstari wa pili na maneno "kuwakilisha" yaliyomo katika mistari ya saba na kumi na mbili katika ibara ndogo ya (4) kama ilivyotajwa upya ili ibara ndogo hiyo isomeke kama ifuatavyo:

"(4) Kwa madhumuni ya kuondoa mashaka juu ya ufafanuzi au utekelezaji wa masharti ya ibara ndogo ya (2) na ya (3) ya Ibara hii, inatamkwa rasmi hapa kwamba isipokuwa kama masharti ya Katiba hii au ya sheria nyingine yoyote yameagiza vingine, Jaji Mkuu atakuwa na uwezo wa kutoa kwa Jaji Kiongozi mara kwa mara maagizo au maelekezo kuhusu utendaji wa kazi na shughuli zake kama Mkuu wa Mahakama Kuu; vile vile, Jaji Mkuu atakuwa na uwezo wa kukasimu kwa Jaji Kiongozi baadhi ya madaraka yake ya uongozi na usimamizi juu ya utekelezaji wa kazi katika

Mahakama Kuu na Mahakama nyinginezo zote za ngazi ya chini yake, na kila inapohitajika, Jaji Mkuu anaweza kutekeleza yeye mwenyewe moja kwa moja madaraka yake yoyote aliyoyakasimu kwa Jaji Kiongozi."

(d) kufuta tarakimu ya "(9 )" na ya "(8)" zilizopo katika mstari wa kwanza na wa tatu na neno "mitano" lililomo katika mstari wa tano wa ibara ndogo ya (6) kama ilivyoitwa upya ili sasa isomeke kama ifuatavyo:

"(6) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (8) ya Ibara hii, mtu aweza tu kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ikiwa ana sifa maalum, kama ilivyofafanuliwa katika ibara ndogo ya (7) ya Ibara hii, na awe mtu ambaye amekuwa na mojawapo ya sifa maalum kwa muda usiopungua miaka kumi."

(e) kufuta tarakimu ya "(7)", "(9)" na ya "(11)" zilizopo katika mstari wa kwanza na wa pili wa ibara ndogo ya (7) kama ilivyotajwa upya na kuweka badala yake tarakimu "(6)", (8)" na ya "(10)";

(f) kuifuta ibara ndogo ya (7) kama ilivyotajwa upya na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(7) kwa madhumuni ya ufafanuzi wa ibara ndogo za (6), (8) na (10) ya Ibara hii, sifa maalumu maana yake ni mtu aliye na shahada ya sheria kutoka chuo kikuu kinachotambuliwa na mamlaka ya ithibati Tanzania na-

(a) amekuwa hakimu;

(b) amefanya kazi katika utumishi wa umma akiwa na sifa za kufanya kazi ya uwakili au ni wakili wa kujitegemea;

(c) ana sifa ya kusajiliwa kuwa wakili,
na, amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi."

(g) kuifuta ibara ndogo ya (8) kama ilivyotajwa upya na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(8) Iwapo Rais atatosheka kwamba ijapokuwa mtu mwenye sifa mojawapo ya hizo sifa maalum hakuwa nayo sifa hiyo kwa muda usiopungua miaka kumi, lakini mtu huyo ana uwezo, ujuzi na kwa kila hali anafaa kukabidhiwa madaraka ya Jaji wa Mahakama Kuu na kuna sababu za kumfanya mtu huyo astahili kukabidhiwa madaraka hayo, basi Rais aweza kutengua lile sharti la kuwa na sifa maalum kwa muda usiopungua miaka kumi na baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi wa Mahakama, Rais aweza kumteua mtu huyo kuwa Jaji wa Mahakama Kuu."

(h) kuifuta tarakimu "(11)" iliyomo katika mstari wa pili wa ibara ndogo ya (11) kama ilivyoitwa upya na kuiweka badala yake tarakimu "(10)";

(i) kuifuta aya ya (b) ya ibara ndogo ya (10) kama ilivyoitwa upya na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(b) kwa madhumuni ya kumteua Kaimu Jaji kwa mujibu wa masharti ya ibara hii ndogo, Rais anaweza kutengua lile sharti la kuwa na sifa maalum kwa muda usiopungua miaka kumi kwa sababu kama zile zilizotajwa katika ibara ndogo ya (8) ya Ibara hii".

Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 110

**18.** Ibara ya 110 inafanyiwa mabadiliko kama ifuatavyo:

(a) Kwa kuifuta ibara ndogo ya (2) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(2) Jaji yeyote wa Mahakama Kuu anaweza kustaafu kazi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wakati wowote baada ya kutimiza umri wa miaka hamsini na tano, isipokuwa kama Rais ataagiza kwamba asistaafu, na iwapo Rais ataagiza hivyo, basi huyo Jaji atakayehusika na maagizo hayo ya Rais hatakuwa na haki ya kustaafu mpaka upite kwanza muda wowote utakaotajwa na Rais kwa ajili hiyo."

(b) kwa kuzifuta ibara ndogo za (5), (6), (7), (8) na (9).

Kuongeza Ibara mpya ya 110A.

**19.** Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuongeza Ibara mpya ya 110A mara tu baada ya Ibara ya 110 kama ifuatavyo:

"Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama Kuu

110A.-(1) Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji, kwa sababu mbali na zile zilizoainishwa katika ibara ndogo ya (2), utakuwa kama utakavyoelekezwa na Sheria itakayotungwa na Bunge.

(2) Jaji wa Mahakama Kuu aweza tu kuondolewa katika madaraka ya kazi kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi yake (ama kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote) au kwa sababu ya tabia mbaya inayoathiri maadili ya kazi ya Jaji au sheria ya maadili ya viongozi wa umma; na hataweza kuondolewa kazini ila kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (4) ya Ibara hii.

(3) Iwapo Rais anaona kuwa suala la kumwondoa Jaji kazini lahitaji kuchunguzwa, basi katika hali hiyo utaratibu utakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Rais anaweza baada ya kushauriana na Jaji Mkuu, kumsimamisha kazi Jaji huyo;

(b) Rais atateua Tume ambayo itakuwa na Mwenyekiti na Wajumbe wengine wasiopungua wawili. Na huyo Mwenyekiti na angalau nusu ya Wajumbe wengine wa Tume hiyo itabidi wawe watu ambao ni Majaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani katika nchi yoyote iliyomo kwenye Jumuiya ya Madola;

(c) Tume hiyo itachunguza shauri lote halafu itatoa taarifa kwa Rais kuhusu maelezo ya shauri lolote na itamshauri Rais kama huyo Jaji anayehusika aondolewe kazini kwa mujibu wa masharti ya Ibara hii kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya.

(4) Ikiwa Tume iliyoteuliwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (3) itamshauri Rais kwamba Jaji ambaye habari zake zimechunguzwa na hiyo Tume aondolewe kazini kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya, basi Rais atamwondoa kazini Jaji huyo anayehusika na utumishi wa Jaji huyo utakuwa umekoma.

(5) Ikiwa suala la kumwondoa Jaji kazini limepelekwa kwenye Tume kwa ajili ya uchunguzi kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (3) ya Ibara hii, Rais anaweza kumsimamisha kazi Jaji huyo anayehusika, na Rais aweza wakati wowote kufuta uamuzi huo wa kumsimamisha kazi Jaji huyo, na kwa hali yoyote uamuzi huo utabatilika ikiwa Tume itamshauri Rais kwamba Jaji huyo asiondolewe kazini.

(6) Masharti ya Ibara hii yatatumika bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (11) ya Ibara ya 109 ya Katiba hii."

**20.** Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuyafuta maelezo ya Sehemu ya Tatu ya Sura ya Tano na kuyaandika upya kama ifuatavyo: Kufanya mabadiliko katika Sehemu ya Tatu ya Sura ya Tano

"SEHEMU YA TATU

TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA

**112.**-(1) Kutakuwa na Tume ya Ushauri wa Uteuzi wa Majaji na Ajira ya Mahakimu wa Mahakama za Tanzania Bara ambayo katika Katiba hii itaitwa "Tume ya Utumishi wa Mahakama". Tume ya Utumishi wa Mahakama

(2) Wajumbe wa Tume hiyo watakuwa:

(a) Jaji Mkuu ambaye atakuwa Mwenyekiti;
(b) Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
(c) Jaji mmoja wa Mahakama ya Rufaa atakayeteuliwa kwa ajili hiyo na Rais baada ya kushauriana na Jaji Mkuu;
(d) Jaji Kiongozi; na
(e) Wajumbe wawili watakaoteuliwa na Rais.

(3) Mtu hataweza kuteuliwa kuwa mjumbe wa Tume kwa mujibu wa masharti ya aya ya (e) ya ibara ndogo ya (2) ya Ibara hii ikiwa mtu huyo ni Mbunge au ni mtu mwenye madaraka ya aina nyingine yoyote iliyotajwa kwa ajili hiyo na sheria iliyotungwa na Bunge."

(4) Katika kutekeleza majukumu yake, Tume yaweza kukasimu kazi zake kwa Kamati mbalimbali zitakazoundwa kwa mujibu wa Sheria itakayotungwa na Bunge.

**113.**-(1) Majukumu ya Tume yatakuwa ni- Majukumu na madaraka ya Tume

(a) kumshauri Rais kuhusu uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu;
(b) kumshauri Rais kuhusu masuala ya nidhamu ya majaji;
(c) kumshauri Rais kuhusu mishahara na maslahi ya majaji;
(d) kumshauri Rais kuhusu uteuzi na nidhamu kwa ajili ya Msajili wa Mahakama ya Rufani na Msajili wa Mahakama Kuu;
(e) kuajiri mahakimu na kusimamia nidhamu yao;
(f) kuunda kamati mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake.

(2) Madaraka ya uteuzi, kudhibiti nidhamu na ya kuwaondoa kazini majaji yatakuwa mikononi mwa Rais kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(3) Madaraka ya uteuzi, kuwathibitisha kazini, kudhibiti nidhamu na ya kuwaondoa kazini Wasajili wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu yatakuwa mikononi mwa Rais.

(4) Madaraka ya kuajiri, kuwathibitisha kazini, kudhibiti nidhamu na kuwaondoa kazini mahakimu wa mahakama za Tanzania Bara yatakuwa mikononi mwa Tume iliyotajwa katika Ibara ya 112.

(5) Bunge linaweza kutunga sheria itakayoweka masharti ya utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Uanachama katika vyama vya siasa.

**113A.** Itakuwa ni marufuku kwa Jaji wa Mahakama ya Rufani, Jaji wa Mahakama Kuu, Msajili wa Mahakama ya ngazi yoyote, hakimu wa ngazi yoyote kujiunga na chama chochote cha siasa, isipokuwa tu kwamba atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika Ibara ya 5 ya Katiba hii."

Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 116

**21.**-(1) Ibara ya 116 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko:

(a) kwa kufuta ibara ndogo ya (1); na

(b) kuzitaja ibara ndogo za (2) na (3) kuwa ibara ndogo za (1) na (2).

Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 118

**22.** Ibara ya 118 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko:

(a) kwa kuifuta Ibara hiyo na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"Majaji wa Mahakama ya Rufani na uteuzi wao.

**118.**-(1) Kutakuwa na Jaji Mkuu wa Mahakama (ambaye katika Ibara zifuatazo kwenye Katiba atatajwa tu kwa kifupi kama "Jaji Mkuu") na Majaji wengine wa Rufani wasiopungua wanne, isipokuwa kwamba kikao maalum cha Mahakama nzima kitakamilika kama kitakuwa na Majaji wa Rufani wasiopungua watano.

(2) Jaji Mkuu atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye sifa za kuwa Jaji wa Rufani na atakuwa ndiye Kiongozi wa Mahakama ya Rufani na pia Mkuu wa Mahakama kama ilivyofafanuliwa katika Ibara ya 116 ya Katiba na atashika madaraka ya Jaji Mkuu mpaka atakapotimiza umri wa kustaafu kama Jaji wa Rufani, isipokuwa kama:

(a) atajiuzulu; au

(b) kiti chake kitakuwa wazi kutokana na maradhi au kifo;

(c) atavuliwa wadhifa wa Jaji Mkuu na Rais.

(3) Majaji wengine wa Rufani watateuliwa na Rais, baada ya kushauriana na Jaji Mkuu, kutoka miongoni mwa watu wenye sifa za kuteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano zilivyoainishwa katika Ibara ya 109 ya Katiba au kutoka miongoni mwa watu wanaoweza kuteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar kwa mujibu wa sheria zinazotumika Zanzibar na wamekuwa na sifa hizo kwa muda usiopungua miaka kumi na tano.

(4) Iwapo itatokea kwamba:-

(a) Kiti cha Jaji Mkuu kitakuwa wazi; au

(b) Jaji Mkuu hayupo Tanzania; au

(c) Jaji Mkuu atashindwa kutekeleza kazi yake kwa sababu yoyote,

na, Rais ataona kuwa kwa muda wa tukio lolote kati ya hayo matatu inafaa kumteua Kaimu Jaji Mkuu, basi Rais anaweza kumteua Kaimu Jaji Mkuu kutoka miongoni mwa Majaji wa Rufani.

(5) Kaimu Jaji Mkuu atatekeleza kazi za Jaji Mkuu mpaka atakapoteuliwa Jaji Mkuu mwingine au mpaka Jaji Mkuu ambaye alikuwa hayupo Tanzania au alikuwa hamudu kazi zake atakaporejea kazini.

(6) Ikitokea kwamba kiti cha Jaji wa Rufani kitakuwa wazi au endapo Jaji wa Rufani yeyote atateuliwa kuwa Kaimu Jaji Mkuu au kama Jaji wa Rufani atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu yoyote, au Jaji Mkuu atamshauri Rais kuwa kazi za Mahakama ya Rufani ilivyo wakati huo zahitaji ateuliwe Kaimu Jaji wa Rufani, basi Rais aweza, baada ya kushauriana na Jaji Mkuu, kumteua Kaimu Jaji wa Rufani kutoka miongoni mwa watu ambao wanaweza kuteuliwa kuwa Majaji wa Rufani kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (4) ya Ibara hii.

(7) Mtu yeyote atakayeteuliwa kuwa Kaimu Jaji wa Rufani ataendelea kufanya kazi kama Kaimu Jaji wa Rufani kwa muda wowote utakaotajwa wakati wa kuteuliwa kwake, au, endapo muda haukutajwa, mpaka uteuzi wake utakapofutwa na Rais, lakini bila ya kujali kwamba muda wake wa kazi umemalizika au kwamba uteuzi wake umefutwa, mtu huyo anaweza kuendelea kufanya kazi kama Kaimu Jaji wa Rufani mpaka amalize kutayarisha na kutoa hukumu au mpaka akamilishe shughuli nyingine yoyote inayohusika na rufaa au mashauri mengine yoyote ambayo alikwishaanza kuyasikiliza kabla ya muda wake wa kazi haujamalizika au uteuzi wake haujafutwa.

(8) Kwa madhumuni ya kuondoa mashaka juu ya ufafanuzi wa masharti ya ibara ndogo ya (1) ya Ibara hii na Ibara ya 119 ya Katiba hii, inatamkwa rasmi hapa kwamba mtu aliyeteuliwa kuwa Kaimu Jaji wa Rufani atakuwa na mamlaka kamili ya Jaji wa Rufani na atatekeleza kazi zote za Jaji wa Rufani na

kwamba idadi ya Majaji iliyotajwa katika Ibara ya 122 ya Katiba hii, haitaathirika kwa sababu tu mmoja au zaidi ya Majaji wa Rufani katika kikao chochote ni Kaimu Jaji wa Rufani.

(9) Ofisi ya Jaji wa Rufani haitafutwa wakati yupo mtu aliyeshika madaraka ya kiti cha Jaji wa Rufani.";

(b) kufuta maneno "ya Tanzania" popote yalipo katika Ibara ya 118.

**23.** Ibara ya 120 inafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:- Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 120

"Muda wa Utumishi wa Majaji wa Rufani

**120.**-(1) Kila Jaji wa Rufani atalazimika kuacha kazi yake atakapotimiza umri wa miaka sitini na tano, lakini masharti ya Ibara hii ndogo yatatumika bila kuathiri masharti yafuatayo katika ibara hii.

(2) Jaji yeyote wa Rufani aweza kustaafu kazi ya Ujaji wa Rufani wakati wowote baada ya kutimiza umri wa miaka sitini, isipokuwa kama Rais ataagiza kwamba asistaafu, na iwapo Rais ataagiza hivyo, basi huyo Jaji wa Rufani atakayehusika na maagizo hayo ya Rais hatakuwa na haki ya kustaafu mpaka upite kwanza muda wowote utakaotajwa na Rais kwa ajili hiyo.

(3) Iwapo Rais ataona kuwa kwa ajili ya manufaa ya umma inafaa Jaji wa Rufani aliyetimiza umri wa miaka sitini na tano aendelee kufanya kazi, na Jaji huyo wa Rufani anakubali kwa maandishi kuendelea kufanya kazi, basi Rais aweza kuagiza kuwa Jaji huyo wa Rufani aendelee kufanya kazi kwa muda wowote utakaotajwa na Rais.

(4) Bila ya kujali kwamba Jaji wa Rufani ametimiza umri ambao analazimika kuacha kazi kwa mujibu wa masharti ya Ibara hii, mtu anayefanya kazi ya Jaji wa Rufani aweza

(b) kufuta na kuandika upya maneno:
"Jaji Mkuu" maana yake ni Jaji Mkuu aliyetajwa, kuteuliwa na ambaye majukumu yake yameelekezwa katika Ibara ya 118 ya Katiba."

(c) Kufuta maneno "Idara ya" katika tafsiri ya maneno "Jaji Mkuu wa Zanzibar" na vile vile katika ibara ndogo ya (2) ya Ibara ya 4 ya Katiba."

Umepitishwa na Bunge tarehe 7 Februari, 2005

DAMIAN S. FOKA,
*Katibu wa Bunge*